# Learning by Ear 2011/2012 – Corruption – The Elephant in the Room

## Episode 06 – "The Truth Must Come Out"

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck, Friederike Müller, Pendo Paul**

**Proofreading: Charlotte Collins, Pendo Paul**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

CHARACTERS:

- NARRATOR

Scene 1:

- Lydia (FEMALE, 16)
- Tekla (FEMALE, 16)
- Ms Tatu, teacher (FEMALE, 43)

Scene 2:

- Jeffrey (MALE, 58)
- Lydia (FEMALE, 16)
- Tekla (FEMALE, 16)
- NARRATOR

Scene 3:

- Jeffrey (MALE, 58)

- Alfayo (MALE, 58)

**Intro:**

**0. Narrator:**

Hujambo na karibu kwa sehemu ya sita ya mfululizo wa vipindi vya **Noa Bongo Jenga Maisha yako**, kwenye mchezo wa redio kuhusu jinamizi ufisadi kwa jina “**Tembo Nyumbani**”.Katika mfulululizo huu wa vipindi kumi, tunafuatilia maisha ya familia ya Odhiambo na rafiki yao Jeffrey Thiongo, katika juhudi zao za kupambana na ufisadi. Katika kipindi kilichotangulia, Jeffrey anazindua rasmi shirika lake la kupambana na ufisadi, la “**Komesha Ufisadi Sasa**” wakati mkutano na waandishi wa habari uliofana. Jeffrey anapigwa na bumbuazi baada ya kuulizwa swali ghafla iwapo anafikiria kujitosa kwenye siasa kugombea kiti cha ubunge. Kwa upande mwengine, Isaac Odhiambo anakumbana na jinamizi la ufisadi ofisini mwake wakati mfanyakazi mwenzake anapojaribu kutumia mbinu za upendeleo kwenye zoezi la kuwaajiri wafanyakazi wapya katika kampuni yao. Katika kipindi cha leo, “**Ukweli lazima Udhihirike**” tutasikia iwapo Alfayo Odhiambo, atakiri hadharani kwamba kampuni yake inahusika na sekta ya nishati. Lakini kwanza tunaungana na Lydia Odhiambo shuleni ambako yeye na rafiki yake Tekla wameamua

kwenda kumuona mwalimu wao kuhusiana na matokeo yao mabaya ya mtihani wa mwishoni mwa mwaka ambayo yamewashangaza.

**Scene One:**

**1. SFX:** **Classroom: Low murmuring, papers rustling**

**2. Ms Tatu:** Haya ndio matokeo ya mtihani wa mwisho wa mwaka!. Tumpigie makofi Jane kwa kuongoza katika mtihani mwaka huu. Pia, wapo wengine waliofanya vyema katika mtihani huo.

**3. SFX:** **clapping**

**4. Lydia:** **(muttering under breath)** Tekla, ni vipi Jane aliweza kupata matokeo mazuri hivi? Kwanza yeye ni mvivu wa hata kushika kalamu! Sijawahi kumuona akifanya kazi zake za shule, wala hata kuinua mkono kuuliza swali darasani.

**5. Tekla:** **(murmuring)** Najua vizuri, na nimeshangaa sana!

***KW begin*** Haiwezekani, na najua kila mmoja anajiuliza swali hili. Na pia ni vipi Samuel aliweza kuwa miongoni mwa wanafunzi kumi bora? Alinishinda hata mimi...! licha ya kwamba kila mmoja anafahamu kuwa yeye ni mbumbumbu darasani!

***KW end***

**6. SFX:** **Chairs scraping, loud chatter. Kids leaving the classroom**

**7. Lydia:** **(to Tekla)** Hebu twende Tekla tukamuulize!

**8. Tekla:** Kumuuliza nani?

**9. Lydia:** Mwalimu wetu Bi. Tatu. Hapa si kuwa na upendeleo wakati wa kusahihisha mtihani...bali kuhakikisha kuwa bidii za wanafunzi werevu darasani zinaonekana.

**10. Tekla:** Ohhh…Lydia! Sijui pengine hatasikia vizuri tukisema kuwa ana upendeleo. Si unajua ana hasira za haraka.

**11. Lydia:** Mimi sijali. Tekla, kila mmoja anajua kwamba wewe ndiye mwanafunzi mwerevu zaidi darasani. Na tulitarajia utakuwa wa kwanza darasani, wala sio Jane. Nitamwambia mwalimu. Twend.

**12. Lydia:** **(clears throat)** Umm, Samahani Bi. Tatu. Tunaweza kukuona ?

**13. Ms. Tatu:** Sawa, Lydia, kuna shida gani?

**14. Lydia:** Bi. Tatu…hili ni suala nyeti, na nisingependa kukuudhi lakini ni vipi Jane alivyoweza kuongoza darasani mwetu na sio Tekla?

***KW Begin***

**15. Ms Tatu:** Unamaanisha nini Lydia? Jane aliweza kupata alama bora zaidi katika mtihani huo.

**16. Lydia:** Nafahamu hilo. Lakini aliwezaje? Hafanyi kazi zake za shuleni, hazungumzi darasani na haonekani akifanya kazi zozote au kutia bidii kwenya masomo. Si wewe mwenyewe unaona hilo ni tatizo Bi. Tatu. Huuhhh?

***KW End***

**17. Ms Tatu**: Unamaanisha nini Lydia?

**18. Lydia:** Sina hakika lakini nilidhani wewe unaweza kutoa ufafanuzi zaidi. Kila mmoja wetu anafahamu kwamba Tekla ni mwanafunzi bora darasani lakini aliweza kushika nafasi ya tano mwaka huu. Inawezekanaje?

**19. Ms Tatu**: Mmmmmm. Saaaaawa. Na wewe mwenyewe, Tekla unasemaje kuhusu matokeo hayo?

**20. Tekla:** Ama kwa hakika, sijaridhika hata kidogo Bi Tatu. Japo sikutarajia kuwa mwanafunzi bora, lakini nafasi ya tano Bi. Tatu...sijawai kushuka chini ya nafasi ya tatu. Na kama Tekla anavyosema tunashuku kuna njama fulani.

**21. Lydia:** Mamangu ni mwalimu katika shule jirani, na wiki iliyopita kulitokea kisa ambapo mzazi wa mwanafunzi mmoja alikwenda kujaribu kumhonga ili mtoto wake aweze kupata alama bora. Je, Bi. Tatu unaweza kuchukua hongo?

**22. Ms. Tatu:** Sikilizeni kwa makini, Mnafahamu mwalimu analipwa mshahara kiasi gani? Au muda anaolazimika kufanya kazi? Ni kweli, mara kwa mara nakubali rushwa kutoka kwa wazazi ili niwasaidie watoto wao. Sina jinsi. Ila hivyo ndivyo mambo yanavyokwenda. Samahani wasichana nataka kurudi kazini. Tuonane kesho!

**23. SFX:** **chair scraping**

**24. SFX:** **door opening and closing**

**25. Lydia:** (**angry)** Nilijua tu. Jambo hili linaniudhi sana! Kuna haja gani ya kutia bidii katika masomo yako kwa muda wa mwaka mzima kisha wazazi wa wanafunzi wengine wavivu wanakuja tu kuwahonga walimu na kupata matokeo ya bure?

**26. Tekla:** Ni jambo linalonikera sana. Tutafanya nini? Tulifichue? Huumm .. tuufichue uovu huu..! Najua si hapa shuleni

kwetu pekee bali hata katika shule nyingine mambo haya yanatokea. Hakuna tofauti!

**27. Lydia:** **(thoughtful)** Hmmm… Tekla, umetoa wazo zuri. Hebu nifuate. Tutafichua kashfa hii. Kwasababu sekta yote ya elimu imeoza kwa ufisadi. Bidii ya mtu haina maana yoyote siku hizi. Twende!

**28. Tekla:** Lydia! Tunaenda wapi?

**29. Lydia:** Kumuona rafiki yetu Jeffrey na dadangu, Sylvia.

**30. Tekla:** Watafanya nini sasa?

**31. Lydia:** Twende katika lile shirika jipya la Jeffrey mjinga wewe! Kwani umesahau mara moja hii? Lile shirika la "**Komesha Ufisadi**". Sylvia anafanya kazi pamoja na Jeffrey. Tutawafahamisha kuhusu ufisadi unaoendelea katika sekta ya elimu. Huoni hilo ni wazo zuri? Sasa twende upesi!

**32. SFX:** **footsteps, door slams**

**End of Scene One**

**33. Narrator:** Watakaposikia habari kuhusu ufisadi unaoendela shuleni kutoka kwa Lydia na Tekla, hapana shaka suala hili halitawashangaza Jeffrey na Sylvia. Ufisadi umekuwa jambo la kawaida, japo hakuna mtu hata mmoja amethubutu kulizungumzia hadharani. Lakini sasa Jeffrey anataka kulivalia njuga suala hili, ili kuchunguza ufisadi unaoendelea miongoni mwa walimu shuleni. Hata hivyo, lakini atahitaji msaada wa Tekla na Lydia kama mashahidi.

## Scene Two:

**34. Atmo:** **Office noises**

**35. Jeffrey:** Sawa, Lydia na Tekla: Niko tayari kuchunguza kesi hii. Naamini ufisadi huu sio tu umekithiri shuleni mwenu bali katika shule zote kote nchini. Lakini cha msingi ni kupata ushahidi wa kutosha.

**36. Lydia:** Sasa tutaanzia wapi, Jeffrey?

**37. Jeffrey:** Lydia ni kufanya uchunguzi wa kina kama majasusi. Nitawapa vifaa na msaada wote mnaouhitaji.

**38. Tekla:** Nadhani sasa tutaanza kuona mwangaza...! Unataka twende kunasa sauti ya Bi. Tatu, akikiri kwamba anachukua hongo, sivyo?

**39. Jeffrey:** Hasa, Tekla. Unaweza kufanya hivyo?

**40. Lydia:** Tunaweza, wacha tujaribu.

**41. Tekla:** Ohhh Mungu wangu. Na je, tukishikwa? Tutashtakiwa?

**42. Jeffrey:** Ehhhh… usiwe na wasiwasi. Hatutashikwa. ..sawa? **(laughs encouragingly)** Lakini lazima uwe muangalifu. Mtatekeleza jukumu hili kwa pamoja. Hakikisheni mnazungumza na mwalimu wenu akiwa peke yake, hasa akiwa darasani. Hataweza kushuku chochote! Mko tayari kwa kazi hiyo? Najua mko tayari si lazima niulize...

**43. Tekla:** Ndio tuko tayari. Lakini naogopa.

**44. Jeffrey:** Sawa kabisa. Najua kwamba nyinyi ni wasichana majasiri. Mtaandamana na Sylvia ili aweze kuwapa vifaa vya kunasa sauti, na kuwaonesha jinsi ya vinavyofanya kazi. Sawa? Kila la kheri!

**End of Scene Two**

**45. Narrator:** Kama tu uamuzi uliochukuliwa na Lydia, rafiki yake na Jeffrey, kwa upande wake naye Alfayo hatimaye anaamua kuwa jasiri na kufika katika shirika hilo la **Komesha Ufisadi Sasa**. Lakini kashfa anayoiwasilisha kwa shirika hili si jambo geni kwa Jeffrey. Amewahi kumpasha habari Jeffrey ambaye alikuwa akifuatilia uchunguzi kuhusu kashfa wakati alipokuwa akihudumu kama mwanachama wa Halmashauri ya Kupambana na Ufisadi.. Ameamua kufanya hivyo, kwasababu kampuni yake imehusika pakubwa katika sakata hili. Jeffrey anakubali kukutana na Alfayo katika mgahawa mmoja ili kupokea taarifa yake rasmi.

## <u>Scene Three</u>

**46. Atmo:** **Café noises**

**47. Jeffrey:** Unajihisi vipi Bw.Alfayo Odhiambo? Je uko tayari kukabiliana na suala hili?

**48. Alfayo:** **(ashamed)** Nimekuwa nikijiuliza masuali kama kweli nimekupata vizuri uliponiuliza tukutane kwenye mghawa

huu badala ya kituo cha polisi ambako ni rahisi maofisa wa polisi kunitia pingu**....**

**49. Jeffrey:** **(laughing**) Hata sikufikiria hilo... **(roar of laughter)** Hapana siwezi kufanya hivyo. ..! Nimeonelea bora tukutana mahali hapa kwasababu binti yako Sylvia tunafanya kazi na yeye, na hana habari kwamba kampuni yako inahusika katika sakata hili.

**50. Alfayo:** Wazo zuri sana. Na sio yeye tu familia yangu yote haina habari. Kwa hakika watashangaa…! **(sighing)** Kwani nimefanya nini kujikuta katika balaa hili lote? Nitasema nini kwa Jeniffer? Nimewaaibisha sana, Jeffrey!

**51. Jeffrey:** Nisikilize, Alfayo. Usijilaumu. Hatimaye watakuja kukuelewa. Wewe si fisadi; hukujua ni mtego gani uliokuwa ukiuingia, lakini furaha yangu nikuona kwamba sasa unafanya jambo la busara. Tunahitaji taarifa zako. Tayari tuna ushahidi wa kutosha dhidi ya waziri wa nishati na washirika wake, lakini hatujapata mtu anayeweza kutoa ushahidi dhidi yao. Una uhakika utaweza kutoa ushahidi katika sakata hili?

**52. Alfayo:** Usiniulize tena swali hilo naweza kubadilisha nia yangu. Kwa hakika nimekuwa nikilifikiria jambo hili kwa muda mrefu sana na sasa sioni ni vipi naweza kubadili msimamo huu. Nafahamu wananiandama sana baada ya kukataa kuwasaidia katika mipango ya kufadhili kampeni zao. Unajua juhudi zangu zote nilikuwa nimezielekeza katika kandarasi hizi kubwakubwa. Bila ya wao mimi na kampuni yangu ningeporomoka. Na zaidi wamenichafulia jina. Nataka pia kuwaona nao wakiporomoka!

**53. Jeffrey**: Sawa kabisa. Tutawapata tu. Lakini lazima ujiandae kwa kuwa na wakati mgumu. Kupiga kipenga ni rahisi lakini kumbuka bado kuna kibarua mbele yetu. Sisi ni marafiki na daima tutadumisha urafiki wetu.

**54. Alfayo:** Asante sana, Jeffrey.

**55. Jeffrey:** Sawa, sasa tunaweza kutia sahihi stakabadhi hizi, na kisha... .maisha yako sasa yako mikononi mwetu. **(laughing)** Usiwe na hofu Alfayo, hatimaye mambo yatakuwa sawa, nakuhakikishia hilo.

**End of Scene Three**

**MUSIC (FADE UNDER OUTRO)**

**56. NARRATOR:** Na kufikia hapo ndipo tunapokamilisha makala haya ya sita katika mfululizo wa mchezo huu wa redio kuhusu Ufisadi, kwa jina "**Tembo Nyumbani**".

Alfanyo anakabiliwa na wakati mgumu, lakini kwa ushirikiano wa rafiki yake Jeffrey amejitolea kusimama wima kupambana na ufisadi. Lakini hata hivyo, anafahamu kwamba haitakuwa kazi rahisi. Je, Lydia na Tekla watafaulu kurekodi sauti ya mwalimu wao? Watafanikiwa kunasa sauti yake akikiri kuchukua rushwa?

Ungana nasi kwenye makala yajayo usikie yatakayojiri. Ukipenda kukisikiliza tena kipindi hiki tembelea mtandao wetu dw.de/lbe, na pia ukiwa na maoni unaweza kuwasiliana nasi kupitia ukurasa wetu wa Facebook. Ni hayo tu kwa leo hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.